



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**MWALIKO KWA WATAZAMAJI WA NDANI KATIKA ZOEZI LA
UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwezi Juni, 2019.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 40(1) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2018 (zilizoandaliwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2018 (zilizoandaliwa chini ya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292), Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kutoa mwaliko kwa Watazamaji wenye nia ya kutazama zoezi hilo.

Kupitia tangazo hili, Tume inapenda kualika maombi kutoka Taasisi na Asasi mbalimbali ambazo zinahitaji kutazama zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Taasisi na Asasi zenye nia ya kuwa Watazamaji wa Uboreshaji zinatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Ofisi za Tume kuanzia tarehe 02 Mei, 2019 na mwisho wa kupokea maombi hayo itakuwa ni tarehe 20 Mei, 2019.

Barua ya maombi itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo:-

- (i) Anuani kamili ya Taasisi/Asasi husika.
- (ii) Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi/Asasi husika.
- (iii) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi/Asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili.
- (iv) Majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi/Asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili.
- (v) Ikiwa Taasisi/Asasi inahusisha Watendaji wa Kimataifa, wawili lazima wawe Watanzania.

- (vi) Kuambatisha nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi/Asasi husika.
- (vii) Kuambatisha nakala/kivuli cha Katiba ya Taasisi/Asasi husika.
- (viii) Maeneo ambayo Taasisi/Asasi inataka kufanya zoezi la Utazamaji.
- (ix) Idadi ya watu ambao Taasisi/Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.

Tume baada ya kupokea barua za maombi itazitaarifu Taasisi/Asasi husika iwapo zimekubaliwa au kukataliwa.

Imetolewa na;

MKURUGENZI WA UCHAGUZI